



SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2
SOUAHLÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2
SUAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2

Tuesday 23 May 2006 (afternoon)

Mardi 23 mai 2006 (après-midi)

Martes 23 de mayo de 2006 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3^e partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2^e partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3^e partie n'obtiendront pas une note élevée.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Jibu suala moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi ya sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo amba umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nyngi.*

Tamthilia

1. Ama

- (a) Kwa kuzingatia kazi mbili ulizojitayarishia, jadili jinsi mwandishi anavyowaumba wahusika wawili na jinsi anavyowatumia katika kupitisha ujumbe wake. Onyesha jinsi wahusika hawa walivyofaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi.

Au

- (b) Swala la dhuluma na maonevu limeshamiri sana kwenye jamii mbali mbali. Jadili kauli hii ukitoa mifano mwafaka kutokana na tamthilia mbili ulizosoma.

Riwaya

2. Ama

- (a) Kila riwaya sharti iwe na utangulizi, ukuaji, upeo wa juu au upeo wa chini. Kwa kuzingatia kazi mbili ulizosoma, onyesha jinsi ploti anayotumia mwandishi katika kazi zake inavyoonyesha ujuzi na ubunifu katika utunzi wake.

Au

- (b) Mwandishi wa riwaya hutumia mbinu tofauti kuwasawiri wahusika wake. Kwa kuzingatia kazi mbili ulizosoma, jadili mtindo aliotumia mwandishi katika kuwasawiri wahusika wake na uonyeshe vile alivyofaulu.

Ushairi

3. Ama

- (a) Mashairi huchukua mitindo na miundo tofauti. Huku ukizingatia kazi mbili ulizozisoma, jadili kauli hii ukizingatia jinsi mitindo na miundo hii inavyofaa na kuleta mvuto unaostahili kwa msomaji.

Au

- (b) Jadili kwa mapana na marefu maudhui muhimu yanayojitokeza kwenye diwani zozote mbili ulizozisoma. Onyesha vile mwandishi anavyofaulu kukuza maudhui haya na mitindo anayotumia ili kufanikisha uendelezaji wa maudhui haya.

Riwaya ya Mapenzi

4. Ama

- (a) Mapenzi huhitaji kupaliliwa na kujengewa ngome madhubuti. Dhibitisha kauli hii ukionyesha mfano wa mapenzi yaliyoshamiri na yaliyozorota huku ukitoa sababu za kila mojawapo kwa kuzingatia kazi zozote mbili ulizozisoma.

Au

- (b) Kwa kuzingatia kazi mbili za riwaya ulizosoma jadili kuhusu mvutano na utata unaojitokeza kati ya vijana na wazee kuhusu swala la ndoa. Jadili na ulinganishe njia mbalimbali zinazoleta tofauti hizi.

Maswali ya Kijumla

5. Ama

- (a) Matumizi ya lugha yenyе madoido na ulimbwende ni nyenzo muhimu katika fasihi bunifu. Jadili kauli hii huku ukionyesha jinsi waandishi wa kazi ulizosoma wanavyofaulu na kushindwa kutekeleza kauli hii.

Au

- (b) Kwa kutoa maoni yako, jadili jinsi fasihi inavyohusika katika kuongoza na kukuza jamii kimaandili. Fafanua ni kwa njia na vipengele VIPI wasanii wamefaulu kufanya hivi kwa kutoa mifano kutoka kwa kazi ulizozisoma.

Au

- (c) “Tamaa mbele mauti nyuma.” Dhibitisha msemo huu ukirejelea wahusika wawili katika kazi ulizozipitia katika sehemu hii na uonyeshe jinsi walivyotumiwa na mwaandishi kudhibisha kauli hii.

Au

- (d) Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kwa kazi ulizosoma, jadili tabia za wahusika wawili na uonyeshe jinsi wanavyochorwa kama kielelezo madhubuti cha wahusika halisi katika jamii. Je! kuna uwezakano wahusika hawa ni wa kifasihi tu na hawana nafasi katika jamii.